# HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA

**SHULE YA SEKONDARI NKUMBA**
**S.L.P 1370,**
**TABORA.**

____________________

**MZAZI WA ----------------------------------------------**
**S.L.P ------------------------------**
**-----------------------------------**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKUMBA ILIYOKO KATIKA MANISPAA YA TABORA MKOA WA TABORA MWAKA --------------**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka -------------, Shule ya Sekondari Nkumba ipo umbali wa Km _______ Kask/Kus/Mash/Magh mwa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.
Usafiri wa basi kutoka Tabora ni Tsh __________ muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe _____________________. Unatakiwa uripoti shuleni kuanzia tarehe _________________ mwisho wa kuripoti ni tarehe ________________________ (ndani ya siku saba). Baada ya hapo ambao hawajaripoti wote majina yao yatapelekwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare ya Shule

(a) Sare ya shule kwa wavulana wa kidato cha kwanza wote ni **suruali (2)** zenye mifuko mitatu na rinda mbili za mbele, pamoja na mkanda wa ngozi mweusi, kwa wasichana wote sare ni **sketi (2)** zenye **rinda za kuhesabu** zinazovuka magoti kwa inchi nne. Kwa jinsi zote kitambaa sharti kiwe kizito chenye **rangi ya Kijani mgomba.**

(b) Kwa jinsi zote njoo na **shati nyeupe (2) za mikono mifupi.** Kitambaa kiwe tetron, shati liwe na mfuko mmoja na isibane wala isiwe fupi kusudi iwe rahisi kuchomekea

*(c)* Rangi ya **Hijabu nyeupe** na msichana akinyoosha mikono akiwa amesimama mikono ifuniifunikwe na nusu kanzu. Juba za kufunika kichwa pekee hazikubaliki.

*(d)* Socks (2) kwa **jinsia zote** ni **rangi nyeupe** ambazo ni ndefu (stocking), na **viatu** kwa jinsia zote ni vya rangi nyeusi, vya ngozi na vinavyofungwa kwa kamba. Tai kwa jinsia zote sharti iwe ya ***rangi kijani mgomba (uniform).***

(e) Rangi ya michezo kwa shule hii ni ______________________________________ na __________________________________ na viatu vya raba kwa wavulana na wasichana

(f) Sweta zitakazo valiwa wakati wa baridi ni za mikono mirefu zenye **rangi ya kijani mgomba**

(g) Wasichana hawaruhusiwi kufuga nywele, kusuka wala kupaka rangi kucha, wasichana wote na wavulana sharti nywele zao ziwe fupi. Kunyoa kipara haikubaliki.

**2.2 Daftari _______________, kalamu na mkebe wa hisabati na vifaa vya lazima**

**2.3 Mahitaji mengine muhimu:** kwa kuwa shule hii ni ya kutwa, kama mwanafunzi atapangishiwa chumba sharti mzazi wake ahakikishe kuwa anampatia mahitaji muhimu ya kibinadamu na kuhakikisha kuwa anafuatilia maendeleo yake mara kawa mara.

**3.0 Sheria na kanuni za shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya **Elimu Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo *rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995*. *Aidha, inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi,Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi* yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais - **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine, na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli nje na ndani ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za shule

**3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-**

(i) Wizi (ii) Uasherati na Ushoga (iii) Ubakaji (iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, kubeli na kadhalika (v) Kupigana au Kupiga (vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma (vii) Kudharau bendera ya Taifa (viii) Kuwa mjamzito/ kupata mimba (ix) Kuoa au Kuolewa (x) Kutoa mimba (xi) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu (xii) Kukataa adhabu kwa makusudi (xiii) Kuwa na simu ya mkononi (xiv) Kuwa mtoro kwa siku 90 au zaidi.

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na mwanafunzi kabla hajapokelewa shuleni ni:-**

a) Fomu ya kupima Afya ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali

***KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKUMBA***

**------------------------------**

**________________________________________**

**Simu na ________________________________**

**MKUU WA SHULE**